

**“Biblia yasemaje?...”**  
**Yesu aliachukuliaje maandiko?**  
**Sehemu ya saba**

“Kisha Ibilisi mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana Imeandiikwa, Atakuagizia malaika wake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, usimjaribu Bwana Mungu wako” Matthew 4:6-7.

Baada ya Yesu kunukuu maandiko ya mamlaka kutoka katika Agano la Kale ili kupambana na jaribu lake la kwanza kupata kuandikwa. Bado Ibilisi hakuwa tayari kumwacha Yesu. Basi, Ibilisi akamchukua Yesu hadi Yerusalem na kumweka juu kinara cha hekalu, Mathayo 4:5. Hapa Ibilisi akahoji uungu wa Yesu Kristo na akamshawishi ajitupe chini. Katika kumshawishi Yesu, Ibilisi aliiutumia vibaya maana ya maneno yanayopatikana katika Zaburi 91:11-12 ili “kuthhibitisha” anachotaka. Maana ya shetani hapa ilikuwa ni kwamba Mungu atawasaidia waaminifu hata kama waaminifu watamjaribu Mungu.

Yesu alijua kuwa Mungu atawasaidia waaminifu. Walakini, pia Yesu alifahamu kuwa ni dhambi kumjaribu Mungu (1 Wakorintho 10:9-11), na Mungu hatamruhusu mtu awaye yote amjaribu (Yakobo 1:13). Kwa hiyo, Yesu alinukuu Kumbukumbu la Torati 6:16 akasema, “Imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako”. Yesu alijua kuwa Mungu huwasaidia walio wake. Pamoja na hayo, Yesu alijua kuwa hatutakiwi kujipeleka kwenye hatari kwa kudhani kuwa atakuja kimuujiza kutuokoa. Katika Kumbukumbu la Torati 6:16 Waisraeli walikuwa na akili ya kudhani kuwa Mungu hawezi kuwafanya chochote. Walikuwa wanamjaribu Mungu na wakaambiya wasifanye hivyo.

Tena, Yesu alitumia maandiko kuhimili jaribu, na ndiposa tena leo twaweza kujifunza kupitia kwa Yesu jinsi ya kutafsiri maandiko. Na huyo ni Yesu akitumia maandiko kuthhibitisha matendo yake. Kama hakukuwa na mamlaka ya kimaandiko kwa Yesu kushiriki jambo fulani aliquwa hashiriki. Nasi, vivyo hivyo, tunatakiwa kutumia maandiko kuthhibitisha matendo yetu. Paulo aliandika waziwazi, “Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Bwana Yesu” Wakolosai 3:17. Maana yake ni kwamba, ni lazima tuthibitishe kila tunachofanya, kupata kibali katika maandiko cha kufanya ili kujua kuwa ni kamili na ni tendo jema (2 Timotheo 3:16,17).

Je, sote, waume kwa wake, tunafuata mfano wa Yesu na kuitumia Biblia ili kuthhibitisha matendo yetu?